**Journal of Linguistics, Literary and Communication Studies**
Vol. 4 No. 1 (2025): ISSN (Online): 2957-8477
DOI: https://doi.org/10.58721/jllcs.v4i1.921


# Uchunguzi wa Usawiri wa Nadharia ya Udhanaishi katika Misemo ya Kiswahili

**Hadija Jilala**
*Chuo Kikuu Huria cha Tanzania*

## Article History
*Received: 02.10.2024*
*Revised: 28.01.2025*
*Accepted: 30.01.2025*
*Published: 13.02.2025*

## *Keywords*
*Kifo*
*Maisha*
*Misemo*
*Nadharia*
*Udhanaishi*

## How to cite:
Jilala, H. (2025). Uchunguzi wa Usawiri wa Nadharia ya Udhanaishi katika Misemo ya Kiswahili. *Journal of Linguistics, Literary and Communication Studies,* 4(1), 11-22.

*Copyright © 2025*
CC BY NC SA

**Ikisiri**
Makala hii inachunguza usawiri wa Nadharia ya Udhanaishi katika misemo ya Kiswahili. Nadharia ya Udhanaishi inahoji kuhusu kifo na maana ya maisha. Kila jamii inafungamana na imani, itikadi, mwelekeo na falsafa mahususi. Uhai, maisha na kifo hufasiliwa na jamii kupitia lugha na fasihi ya jamii husika. Swali ambalo tunajiuliza ni je, misemo ya Kiswahili inayotumiwa katika maisha ya kila siku imefungamana na kusawiri Nadharia ya Udhanaishi? Hivyo, makala hii imelenga kuchunguza usawiri wa Nadharia ya Udhanaishi katika misemo ya Kiswahili. Lengo la makala hii ni kubainisha usawiri wa udhanaishi katika misemo ya Kiswahili na maana zake. Data zilikusanywa kwa njia ya usomaji makini na dodoso. Aidha, makala hii imetumia mihimili ya Nadharia ya Udhanaishi katika kuchunguza, kuchambua na kujadili usawiri wa udhanaishi katika misemo ya Kiswahili. Makala hii inajadili kwamba, Nadharia ya Udhanaishi inafungamana na maisha ya kila siku ya jamii ya Kiswahili na inasawiriwa katika misemo inayotumiwa kila siku. Hivyo, watu ni waumini wa udhanaishi bila kujua ama kujitanabiasha kama wadhanaishi kupitia misemo wanayotumia katika kuyasawiri maisha na mazingira yao ya kila siku.

*Translation (English)*

***An Examination of the Portrayal of Existentialism Theory in Swahili Sayings***

***Abstract***
*This article explores the representation of existentialist theory within Swahili sayings. Existentialist theory interrogates the concepts of death and the meaning of life. Distinct beliefs, ideologies, orientations, and philosophies unite each society. Societies interpret life, living, and death through their unique languages and literatures. We ponder whether Swahili sayings employed in daily life inherently reflect existentialist theory. Thus, this article investigates the representation of existentialism in Swahili sayings to understand how existentialism is conveyed. This paper seeks to identify the portrayal of existentialist theory in Swahili*

*sayings and their meanings. The data for this study were gathered through critical reading and questionnaire methods. The paper employs the principles of existentialist theory to examine, analyse, and discuss the depiction of existentialism in Swahili sayings. It posits that existentialist theory is intricately linked to the daily lives of Swahili society and is reflected in the sayings used in everyday contexts. As a result, individuals may believe in existentialism without consciously recognising it or labeling themselves as existentialists, as reflected through the sayings they utilize to depict their daily lives and environments.*

**Utangulizi**

Udhanaishi ni falsafa inayosisitiza kuwepo kwa mtu binafsi, uhuru na uchaguzi (Flynn, 2006; Jha, 2020; Sasan, 2023). Ni mtazamo unaoelezea kuwa, wanadamu hufafanua maana ya maisha yao wenyewe, na kujaribu kufanya maamuzi ya busara licha ya kuwepo katika ulimwengu usio na akili (Heidegger, 2008).

Wataalamu kama vile Njogu na Chimerah, 1999; Wamitila, 2003; Wafula na Njogu, 2007; na Wanjala, 2011 wanakubaliana kuwa udhanaishi ni nadharia inayojadili kuhusu dhana ya Maisha. Kwa mfano, Wamitila (2003) anafasiri udhanaishi kama dhana inayotumiwa kuelezea falsafa ya kuwako na maisha. Dhana hii inatumiwa kueleza maono au mitazamo inayohusiana na hali ya maisha ya binadamu, nafasi na jukumu lake ulimwenguni na uhusiano wake na Mungu. Naye Wanjala (2011) anafasiri udhanaishi kama falsafa au mtazamo wa maisha ulio na kitovu chake katika maswali yafuatayo: Maisha ni nini na yana maana gani kwa binadamu? Ni kwa njia gani mwanadamu anaweza kuyabadilisha maisha yake yaliyojaa dhiki, mashaka na huzuni? Kwa ujumla fasili zote zinasisitiza kuwa udhanaishi ni falsafa inayozungumzia na kuhoji kuhusu maisha, uwepo, uhai na kifo.

Udhanaishi ulianzia kwa wanafalsafa wa Karne ya 19 Søren Kierkegaard na Friedrich Nietzsche, ingawa hawakutumia neno hili katika kazi zao (Copper, 1990; Reynolds, 2006). Sasan (2023) anaeleza kuwa, katika miaka ya 1940 na 1950, watetezi wa uwepo kutoka Ufaransa kama vile Jean-Paul Sartre, Albert Camus, na Simone de Beauvoir waliandika kazi za kitaalamu na za kubuni ambazo zilieneza mada kama vile hofu, kuchoka, kutengwa, upuuzi, uchaguzi, uhuru, kujitolea na upuuzi. Huko Ulaya falsafa hii ilijitokeza zaidi katika kazi za fasihi zilizoandikwa baada ya Vita Kuu vya Pili vya Dunia. Mathalani, kazi za waandishi kama vile J.P Sartre, Samwel Becketle, na Albert Camus. Fasihi iliyotokana na tapo hili ilijulikana kama "Fasihi ya Ubwege" (Copper, 1990). Fasihi ya Ubwege inatilia mkazo unasibu na uduni wa mwanadamu. Ni fasihi inayosawiri picha ya mwanadamu kama kiumbe dhaifu kinachoishi maisha yasiyo na maana katika ulimwengu usio na maana. Katika fasihi ya Kiswahili Nadharia ya Udhanaishi inahusishwa zaidi na mwandishi Euphrase Kezilahabi katika kazi zake za *Rosa Mistika* (1971), *Kichwamaji* (1974), *Dunia Uwanja wa Fujo* (1975), *Nagona* (1990) na *Mzingile* (1991) (Rehak, 2007; Gaudioso, 2014; Rettová, 2016; Kipacha, 2019; Fuluge, 2022).

Uhusiano wa lugha na Nadharia ya Udhanaishi katika Kiswahili ni eneo ambalo limevutia watafiti wa lugha. Tafiti kuhusu lugha na udhanaishi zimeangazia udhanaishi katika lugha, nahau, methali na misemo. Baadhi tafiti hizo ni utafiti wa Etta na Mogu (2012) ambao walichunguza umuhimu wa

methali katika epistemolojia ya Kiafrika; na Mwanjakwa (2024) alichunguza jinsi udhanaishi unavyojitokeza katika hadithi, misemo na methali nchini Malawi.

Hivyo, utalii tuliofanya juu ya Nadharia ya Udhanaishi, ulichochea nia ya kufanya utafiti na kuandika makala hii. Mawazo ya Nadharia ya Udhanaishi yamechangia kujenga tatizo na lengo la utafiti huu. Katika mapitio ya awali ya tafiti zinazohusiana na Udhanaishi katika Fasihi ya Kiswahili, tulibaini kwamba, tafiti nyingi zilizofanyika kuhusu Nadharia ya Udhanaishi zimejikita zaidi katika kuchunguza Udhanaishi katika kazi za Fasihi Andishi ya Kiswahili huku Fasihi Simulizi ya Kiswahili ikipewa fursa finyu. Baadhi ya tafiti hizo ni Rehak, 2007; Gaudioso, 2014; Gaudioso, 2015; Fuluge, 2022; Fuluge, 2024. Tafiti kuhusu uhusiano wa fasihi simulizi hasa eneo la semi na Nadharia ya Udhanaishi katika Kiswahili ni eneo ambalo halijamakinikiwa vya kutosha. Hivyo, tukaona tujiegemeze katika Semi aghalabu Misemo ya Kiswahili kwani semi ina aina nyingi zilizojaa utajiri lugha kama alivyowahi kusema Mulokozi (2017).

Misemo ni kauli fupifupi zinazotumiwa na jamii ili kusisitiza ukweli wa jambo fulani (Mulokozi,1996). Ni mafungu ya maneno yanayotumiwa na jamii fulani ili kutoa msisitizo wa maadili fulani. Misemo husanifu amali za jamii husika na hufunza wanajamii kwa kuelekeza dira na mtazamo unaoendana na itikadi, mazingira na muktadha wa maendeleo ya jamii hiyo (Mulokozi,1996; King'ei & Ndalu, 2007; Kipacha, 2014). Hivyo, utafiti huu ni muhimu kwa sababu, kupitia misemo inayotumika katika maisha ya kila siku, muktadha, mazingira na utamaduni wa lugha ya Kiswahili tutaweza kubaini usawiri wa udhanaishi katika Kiswahili. Aidha, utatusaidia kuonesha jinsi Waswahili wanavyotumia misemo kuelezea mapambano yao kuhusu maisha, matatizo, shida hofu zao na kila kitu kinachowakabili katika maisha.

**Nadharia ya Udhanaishi**

Kwa mujibu wa Egbekpulu (2022), Nadharia ya Udhanishi ni falsafa inayoshughulikia masuala kuhusu maisha. Ni mtazamo unaokagua kwa upembuzi hali na nafasi ya mtu katika ulimwengu anaoishi. Huzungumzia uhusiano uliopo baina ya mtu na Mungu wake, na iwapo binadamu anapaswa kuamini kuwepo kwa Mungu (Cooper, 1990; Reynolds, 2006). Sasan (2023) anasema Nadharia hii ilijitokeza mwishoni mwa karne ya 19 na mwanzoni mwa karne ya 20 ikisisitiza uzoefu wa mtu binafsi katika maisha na kuutafuta ukweli.

Nadharia ya Udhanaishi inahusishwa na mwanafalsafa Socrates kupitia kauli yake ya jitambue (know thyself) mwanafalsafa wa Kidenishi Soren KierKegaard na wanafalsafa wa Kijerumani Friedrich Nietzsche, Martin Heidegger na Gabriel Marcel. Aidha, Earnshaw (2006) anamtaja mwanafalsafa Soren Kierkegaard (1813-1855) kama baba wa Udhanaishi anayejitanabaisha kupitia maandiko yake ya: *Fear and Trembling* (1843), *The Concept of Dread* (1844) na *The Sickness unto Death* (1849). Kwa mujibu wa KierKegaard (1843), mtu haishi kwa nguvu zake mwenyewe kwa sababu kuna nguvu zaidi zinazomtawala ambazo ni nguvu za Mungu. Katika kuishi kwake, binadamu hutenda dhambi, na ili aweze kupata utulivu wa nafsi (kiroho) inabidi atubu dhambi hizo. KierKegaard anasisitiza kwamba, binadamu ni kikaragosi cha nguvu zilizomuumba, na katika kuzicha nguvu hizo binadamu hupata utulivu wa kiroho. Hivyo, udhanaishi ni dhana ya hofu pale ambapo binadamu huogopa adhabu kutoka kwa Mungu. Kwa hiyo, binadamu amegubikwa na wasiwasi na hataki kumkosea Mungu na kuhimiza ubinafsi wa binadamu.

Akinbode (2023) anasema, Nadharia ya Udhanaishi ni falsafa inayohusu tafakuri ya kina kuhusu maisha, nafasi ya binadamu ulimwenguni, na uhusiano wake na Mungu. Inachunguza iwapo binadamu anapaswa kuamini uwepo wa Mungu na jinsi imani hiyo inavyoathiri maisha yake ya kila siku. Baadhi ya wanaudhanaishi kama vile Soren Kierkegaard wanaamini uwepo wa Mungu huku wengine kama vile Friedrick Nietzsche, Martin Heidegger, Gabriel Marcel na Karl Jaspers) wakikosa

kuamini kuhusu uwepo wa Mungu. Aidha, kuna kundi la tatu la wale wasiokuwa na uhakika wa kuwepo kwa Mungu kama vile Jean Paul Satre (Wafula na Njogu, 2007; Wamitila, 2003). Makala hii imezingatia kundi la kwanza linaloamini kuhusu kuwepo kwa Mungu. Nadharia ya Udhanaishi inasaidia kuhakiki maisha ya mwanadamu anayeishi katika ulimwengu uliojaa mateso, shida na matatizo mbalimbali yanayosababishwa na binadamu mwenyewe. Miongoni mwa shida hizo ni matatizo ya vita, njaa, uchumi, ndoa, mapenzi, kukosa kazi na ajali barabarani. Matatizo haya humfanya binadamu akose furaha na kukata tamaa kuhusu maisha na hatimaye kushindwa kuelewa sababu ya kuwepo kwake na uwepo wa Mungu.

Kwa mujibu wa Søren Kierkegaard (1941), Jean Paul Sartre (1947) na Camus (1955) nadharia hii imejengeka katika mihimili saba (7). Mihimili hiyo ni: (i) uhuru wa mtu binafsi, (ii) kifo, (iii) suala la Mungu, (iv) utamaushi, (v) ukengeushi, (vi) kuabudu mahitaji ya kimwili, na (vii) utupu wa maisha ama ombwe.

Kuhusu uhuru wa mtu binafsi, wadhanaishi wanaamini kuwa hakuna mtu anayepangiwa jinsi ya kuishi. Na kwamba, mtu mwenyewe ndiye mwenye maamuzi ya kujitafutia maana ya maisha yake kwa kuwa mwanadamu si chochote isipokuwa atakavyoamua mwenyewe kuwa (Sartre, 2018). Hivyo, uhuru wa mtu binafsi, uwezo wa mtu wa kujifikiria na kujiamulia ni wajibu wa binadamu katika ulimwengu. Kwa kuwa, kuna uhuru wa kufanya uamuzi na uamuzi wa kuwa huru. Kwa kuwa, mwanadamu yuko huru kufanya maamuzi yoyote, ila maamuzi yake yanaweza kumfanya azidi kuwa huru au afungike zaidi (Wamitila, 2003; Wafula & Njogu, 2007). Nalo suala la Mungu, yaani kuwepo au kutokuwepo kwa Mungu, baadhi ya wadhanaishi wanaoamini uwepo wa Mungu, wanashikilia kuwa maisha ya mtu yana maana jinsi yalivyo, na kuwa tunaweza tusielewe ila Mungu mwenyewe anajua maana hiyo. Hivyo mwanadamu asikate tamaa, awe na imani kwa sababu imani kwa Mungu pekee huyapa maisha maana. Hata hivyo, wale ambao hawaamini uwepo wa Mungu wanashikilia kuwa mwanadamu ana jukumu la kutafutia maisha yake maana na kwamba yuko huru kuyapa maisha yake maana yoyote anayotaka yeye kwa kuishi anavyotaka, bila kujali kuwa ataadhibiwa siku ya kiama. Kwao, Mungu alikufa kwa hivyo hakuna wa kuwauliza chochote (Wamitila, 2003; Wafula & Njogu, 2007).

Nacho kifo, udhanaishi hutilia mkazo matatizo halisi yanayomsibu binadamu. Hujadili hali kama vile kihoro, ufupi wa uhai, fadhaa, mashaka, pekecho, utupu wa maisha na uchovu na jinsi zinavyoathiri maisha ya binadamu. Jazanda zinazoashiria kiungulia, uchovu, pekecho na kiwewe zinatumika kusawiria hali ya binadamu (Suastra na wenzake, 2024). Mwisho, huangazia kwa hamasa tanzia iliyokurubiana na maisha ya binadamu. Huonyesha kwamba juhudi za mtu za kujitafutia maana ya maisha mara nyingi huishia katika mvunjo au uvunjikaji wa juhudi hizo, hasa katika mauti; wakimaanisha mwisho wa binadamu ni kifo. Hivyo, kifo ni ithibati tosha kuwa maisha hayana maana kwa namna yalivyo (Wamitila, 2003; Wafula & Njogu, 2007).

Ukengeushi unatazamwa kama mtengo au mbanduko au kuhisi ugeni. Hali hii hutokea katika mahusiano mbalimbali katika jamii. Mtu binafsi katika jamii hana nafasi ya kujiamulia matendo yake badala yake analazimika kutenda kulingana na kaida fulani maalumu zilizopangwa na jamii pana. Hivyo, Ukengeushi huanza pale mtu anapojaribu kufikiria kibinafsi na kutenda kinyume na kaida na miiko iliyozoeleka. Huanza kuwa na migogoro ya ndani kwa ndani anapopambana na nguvu hatari ambazo zinajaribu kummeza na kumwangamiza. Matokeo yake, mtu husika hujikuta anajiamulia matendo yake. Mtanziko huu hutokana na harakati za mtu katika kutafuta uhuru wake wa mawazo na matendo, ndipo binadamu huyo hujikuta pasipo kujua anakengeushwa na ama Mungu, jamaa au familia yake, asili yake na yeye mwenyewe (Wamitila, 2003; Wafula & Njogu, 2007).

Nao utamaushi ni kukata tamaa. Wadhanaishi wanaamini kwamba, ijapokuwa mwanadamu yuko huru kuamua na kuwa chochote anachotaka kuwa, anafaa kujua kuwa uhuru huu una mipaka hasa katika mapungufu ya kimaumbile. Mwanadamu huyo asipogundua mipaka yake na akajaribu kufanya mambo na yasiwezekane kwa ajili ya mapungufu haya, basi huweza kukata tamaa kwa kukosa alichokitaka; hivyo, kushindwa kuyapa maisha yake maana. Mwanadamu anaposhindwa kuyakabili maisha namna yalivyo na kushindwa kujitafutia maana ya maisha yake, basi anaweza kufanya uamuzi pekee alio na uwezo nao, ikiwemo kujitoa uhai (Wamitila, 2003; Wafula & Njogu, 2007).

Kuhusu kuabudu mahitaji ya kimwili, wadhanaishi wanaamini kuwa kwa vile binadamu yuko huru kufanya anachotaka, kwa hiyo ni wajibu wake kushughulikia mahitaji yake ya kimwili kwa njia anayotaka yeye (Sherman, 2007). Hivyo ni sawa mtu kushiriki katika matendo kama zinaa, ngono za jinsia moja, kuwa na wapenzi wengi, kulewa, na kadhalika; ili kukidhi mahitaji ya mwili wake. Kwa wadhanaishi, taasisi kama ndoa si muhimu, mradi tu, mtu anapata mahitaji yake ya kimwili (Wamitila, 2003; Wafula & Njogu, 2007). Aidha, mhimili wa utupu wa maisha, kwa mujibu wa wadhanaishi; mwanadamu si chochote. Kwa sababu, kulingana na wadhanaishi, hakuna hata falsafa moja inayoweza kueleza mwanadamu ni kitu gani hasa. Aidha, kifo kinapokuja humfuta mwanadamu na kumfanya mtupu kisha kumwondoa - asiwepo tena, hivyo kuleta ombwe. Matokeo yake, mduara wa utupu hujikamilisha kikamilifu. Kwani kabla ya kuzaliwa mwanadamu, huwa kuna utupu na baada ya kuondoka huacha nyuma utupu. Kwa hiyo, mwanadamu huwako katikati ya utupu; mbele yake kuna utupu na nyuma yake kuna utupu unaothibitisha maisha ya mwanadamu ni ubatili mtupu (Wamitila, 2003; Wafula & Njogu, 2007).

Hivyo, kutokana na mjadala huo wa mihimili ya udhanaishi makala hii imetumia mihimili sita (6) ya Udhanaishi kuchunguza usawiri wa Udhanaishi katika misemo ya Kiswahili. Mihimili hiyo ni: (i) uhuru wa mtu binafsi, (ii) kifo, (iii) suala la Mungu, (iv) utamaushi, (v) ukengeushi, (vi) kuabudu mahitaji ya kimwili. Aidha, mihimili hii imetumika kuchambua na kujadili misemo ya Kiswahili inavyofungamana na kusawiri Udhanaishi. Uamuzi wa kutumia mhimili sita umezingatoa lengo la makala hii.

## Methodolojia ya Utafiti

Data za makala hii zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya usomaji makini na dodoso. Kupitia mbinu ya usomaji makini, mtafiti alisoma machapisho yanayohusiana na mada. Data za misemo zilikusanywa kwa njia ya dodoso kutoka kwa wanafunzi wa Umahiri katika Kiswahili, darasa la 2023/2024, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Wanafunzi wote 17 waliteuliwa kushiriki katika utafiti huu na kupewa dodoso. Kundi hili lilichaguliwa kwa kutumia mbinu ya uteuzi wa makusudi. Kigezo kilichozingatiwa ni kuwa hawa ni wanafunzi wanaosoma nadharia za fasihi. Hivyo, wataweza kutoa data za kutosha kuhusu misemo ya Kiswahili na kueleza maana ya misemo kwa kuihusisha na Nadharia ya Udhanaishi kutokana na maarifa waliyo nayo. Mkabala wa kitaamuli ulitumika katika ukusanyaji, uchanganuzi, pamoja na utoaji wa matokeo ya data. Hivyo, tulikusanya misemo ya Kiswahili 300. Misemo hiyo iliainishwa na kupangwa katika makundi na kuchambuliwa kulingana na malengo ya utafiti huu pamoja na uhusiano wake na mihimili mahsusi. Haikuwa rahisi kutumia misemo yote tuliyokusanya katika makala hii. Hivyo, tuliteua misemo mitano kushadidia hoja katika kila mhimili. Misemo iliyotumika katika utafiti huu iliteuliwa kwa kuzingatia uhusiano wake na mihimili ya udhanaishi kulingana na malengo ya utafiti huu. Aidha, data ya utafiti huu imewasilishwa kwa njia ya maelezo.

**Usawiri wa Nadharia ya Udhanaishi katika Misemo ya Kiswahili**

Makala hii ililenga kuchunguza usawiri wa Nadharia ya Udhanishi katika misemo ya Kiswahili. Kupitia mbinu ya usomaji makini na dodoso, tulibaini kuwa misemo ya Kiswahili imefungamana na kusawiri Nadharia ya Udhanaishi. Sehemu ifuatayo inajadili kwa kina matokeo ya utafiti kwa kutumia mihimili sita ya Udhanaishi.

***Uhuru wa mtu binafsi***

Uhuru wa mtu binafsi ni mhimili wa udhanaishi ambao unasisitiza imani kuwa binadamu ana uhuru wa kufanya maamuzi na kuamua njia ya maisha yake na jinsi maisha yake yatakavyokuwa (Sartre, 2018). Utafiti huu ulibaini misemo ya Kiswahili iliyofungamana na mhimili huu. Tazama mifano katika Jedwali namba 1 hapa chini.

*Jedwali namba 1: Misemo Kuhusu Uhuru wa Mtu Binafsi*

| Namba | Misemo ya Kiswahili |
|---|---|
| 1. | Kichwa changu ndiyo serikali yangu |
| 2. | Maisha ni kuchagua |
| 3. | Kupanga ni kuchagua |
| 4. | Naishi nitakavyo si mpendavyo |
| 5. | Tusipangiane maisha |

***Chanzo:*** *Data za utafiti (Mei- Septemba, 2024)*

Data katika Jedwali namba 1 inadhihirisha misemo inayosawiri dhana ya uhuru wa mtu binafsi. Mathalani, msemo "*Kichwa changu ndiyo serikali yangu*" unaashiria msisitizo wa uhuru wa mtu binafsi katika maamuzi na utekelezaji wa majukumu ya maisha yake. Neno "kichwa" linaonyesha uzito wa akili na utashi wa mtu binafsi, huku "serikali" ikirejelea uwezo wa kujiongoza. Hivyo, msemo huu unasisitiza kuwa mtu binafsi ndiye msimamizi wa maisha yake. Msemo "*Maisha ni kuchagua*" unasisitiza jukumu la mtu binafsi katika kufanya maamuzi yanayoathiri maisha yake. Uchaguzi unaweza kupelekea maisha mazuri au mabaya kulingana na njia ambayo anaamua kuchagua. Msemo huu umefungamana na mawazo ya Simone de Beauvoir (2018) ambaye anasisitiza kuwa njia pekee ya kukabiliana na uhuru ni kuukubali kama mzigo na pia kama baraka. Hivyo, binadamu ana uhuru wa kupanga maisha ili kuyapa maana. Misemo "*Naishi nitakavyo si mpendavyo*" na *"tusipangiane maisha"* ina maana kuwa mtu ana uhuru wa kuamua namna ya kuishi bila kufuata matarajio ya wengine. Hivyo, maisha ya mwanadamu hayapangwi na jamii, bali yanatokana na maamuzi yake binafsi. Kama anavyoeleza Sartre (2018:571) kuwa binadamu anahukumiwa kuwa huru.

Kama inavyobainika katika mjadala hapo juu, misemo ya Kiswahili inasawiri mtazamo wa udhanaishi kuhusu uhuru wa mtu binafsi; kwamba binadamu hutengeneza maana ya maisha yake kupitia maamuzi yake binafsi. Sartre (1957: 293) kama alivyonukuliwa katika Akinbode (2023: 1) anasema "Mwanadamu amehukumiwa kuwa huru; kwa sababu mara tu anapotupwa ulimwenguni, anawajibika kwa kila kitu anachofanya. Ni juu yake kutoa maana ya maisha na matamanio anayofuata, hata yale ya tamaa, bila kujificha nyuma ya uhalali wowote wa nje". Fundisho la uhuru la Sartre ni la kimapinduzi, akipendekeza kwamba watu wakubaliane bila masharti wanapochukua jukumu la maisha yao wenyewe. Aidha, Sartre (2008: 455) anaeleza kuwa "Uhuru ni kile unachofanya kwa kile ulichofanyiwa". Hapa anasisitiza kwamba uhuru haupo tu katika hali ya nje, bali pia unahusiana na uwezo wa mtu wa kuamua jinsi ya kukabiliana na mazingira aliyorithi au aliyomo. Kwa ujumla, misemo ya Kiswahili inathibitisha kiini cha falsafa ya Udhanaishi kuhusu uhuru wa mtu binafsi, jukumu la kufanya maamuzi, na maana ya kuwajibika kwa maisha yake mwenyewe. Suala la uhuru wa mwanadamu limejadiliwa katika Suastra na wenzake (2024) ambao wanaelezea jinsi mawazo ya wadhanaishi yaavyotumika katika lugha za Indonesia na kuelewa maana ya maisha na uhuru binafsi.

***Swala la Mungu***

Wadhanaishi wanajadili suala la Mungu katika mitazamo miwili tofauti. Wapo wanaoamini uwepo wa Mungu na wale ambao hawaamini uwepo wa Mungu. Utafiti huu ulibaini misemo ya Kiswahili ambayo inafungamana na mhimili wa udhanaishi kuhusu swala la uwepo wa Mungu.Tazama mifano katika jedwali lifuatalo:

*Jedwali namba 2: Misemo kuhusu Uwepo wa Mungu*

| Namba | Msemo wa Kiswahili |
|---|---|
| 1. | Mungu ndiye mjuzi wa kila jambo |
| 2. | Mungu ndiye mpangaji wa kila jambo |
| 3. | Mungu ndiye tegemeo langu |
| 4. | Mungu si Athumani |
| 5. | Mungu yupo |

***Chanzo:*** *Data za utafiti (Mei- Septemba, 2024)*

Misemo katika Jedwali 2 inasawiri mtazamo wa jamii ya Kiswahili kuhusu nafasi ya Mungu katika maisha ya binadamu. Msemo "*Mungu ndiye mjuzi wa kila jambo*" unasawiri imani kuwa Mungu anafahamu kila kitu kuhusu maisha ya binadamu. Msemo "*Mungu ndiye mpangaji wa kila jambo*" unasawiri imani kwamba kila kitu katika maisha ya binadamu kimepangwa na Mungu. Kwa upande mwingine, msemo "*Mungu ndiye tegemeo langu*" unasisitiza kuwa mwanadamu anapaswa kumtegemea Mungu kama msingi wa maisha yake. Msemo huu umefungamana na wazo la Kierkegaard (1941) kama alivyonukuliwa na Moore, (2002) anasisitiza kuwa "Jambo ni kujielewa katika uhusiano ulionao na Mungu". Unasisitiza uhusiano wa karibu kati ya mwanadamu na Mungu, ambapo mtu binafsi anatakiwa kumtegemea Mungu kama chanzo cha matumaini na maana katika maisha yake. Msemo "*Mungu si Athumani*" unasisitiza kwamba Mungu hafananishwi na binadamu, akionyesha upekee wa Mungu katika jamii ya Kiswahili. Aidha, msemo "*Mungu yupo*" unawapa wanajamii imani kuwa Mungu yupo na anaweza kuondoa taabu, shida, na huzuni za maisha. Suala kuhusu uwepo wa Mungu linaambatana na mawazo ya mwanaudhanaishi Kierkegaard (1997:114) "Umilele wa Mungu ni wakati wa milele; Hana wakati; Ana umilele". *M*isemo hii inaonyesha nafasi ya Mungu katika maisha ya mwanadamu, kwa kubainisha jinsi imani na uhusiano na Mungu vinavyoweza kuleta maana na mwelekeo katika maisha ya mwanadamu kama ilivyo katika udhanaishi. Suala la uwepo wa Mungu limejadiliwa pia na wahakiki wa Udhanaishi katika falsafa ya Kiafrika. Mfano, Akinola (2022) akijadili suala la uwepo wa Mungu katika falsafa ya Kiafrika anasisitiza kuwa mazingira asilia ya mwanadamu hayawezi kutenganishwa na uwepo wa Mungu. Anaendelea kusisitiza kuwa kila kitu kwenye maisha kinadhibitiwa na Imani mahususi. Mungu ndiye muumba wa miungu, watu na ulimwengu.

***Kifo***

Kifo ni suala ambalo limejadiliwa na waumini wa Nadharia ya Udhanaishi. Katika utafiti huu, tulibaini misemo ya Kiswahili ambayo imefungamana na Nadharia ya Udhanaishi kuhusu suala la kifo. Tazama jedwali lifuatalo:

*Jedwali namba 3: Misemo Kuhusu Dhana ya Kifo*

| **Namba** | **Msemo** |
|---|---|
| 1. | Sote ni maiti watarajiwa |
| 2. | Hakuna dawa ya kuzuia kifo |
| 3. | Kifo ni fumbo |
| 4. | Kifo hakina huruma |
| 5. | Kifo hakikimbiwi |

***Chanzo***: *Data za utafiti (Mei- Septemba, 2024)*

Mifano katika jedwali namba 3 hapo juu inasawiri mhimili wa Nadharia ya Udhanaishi kuhusu kifo. Katika vitabu vya *Fear and Trembling* (1843), *The Concept of Dread* (1844), na *Sickness unto Death* (1849), Kierkegaard anasisitiza kwamba, binadamu ni kikaragosi cha nguvu zilizomuumba na za kijamii. Huyaona maisha ya mtu kuwa ni ya kitanzia na hayana maana, kwa kuwa mwisho wa mwanadamu ni kifo. Kila mtu atakufa bila kujali cheo, madaraka, elimu, utajiri au umaskini (Akinola, 2022). Msemo *"sote ni maiti watarajiwa"* unadhihirisha kwamba hakuna mtu ambaye hatapitia kifo, Msemo huu unaothibitisha hali ya kutokuwa na uhakika wa maisha unaambatana na mawazo ya Heidegger (1927) kama alivyonukuliwa katika Heidegger (2008:306) anayesema, "Kuelekea kifo ndio ukweli wa hali ya juu". Msemo *"Kifo ni fumbo"* unatumika kuonesha kuwa hakuna ajuaye siri ya kifo. Pamoja na kuwa kifo ni kama adhabu kwa mwanadamu kifo humjia mtu siku na wakati asioujua. Ni hali ambayo haiepukiki; kifo hakizuiliki na hakuna dawa inayoweza kuzuia kifo kama ambavyo inaelezwa katika msemo wa Kiswahili *"hakuna dawa ya kuzuia kifo"*. Aidha, kifo hakichagui kama inavyodhihirika katika msemo *"kifo hakina huruma"* Kinaweza kumchukua hata yule unayemtegemea kama nguzo na msaada wako. Isitoshe, binadamu hawezi kukimbia kifo kwa sababu humkumba sehemu na mahali popote kwa muda wowote kama inavyobainika katika msemo *"kifo hakikimbiwi"*.

Kwa ujumla data ya misemo iliyowasilishwa inadhihirisha imani ya wadhanishi kuwa juhudi za mtu binafsi kujisaka au kupambana na maisha huishia katika mauti. Kifo ni uthibitisho wa kutosha kwamba maisha yana mwisho na hayana maana kwa namna yalivyo. Kierkegaard (1993: 179) anasema, "Hali ya uchungu zaidi ya kuwapo ni kukumbuka siku zijazo, haswa ile ambayo hautawahi kuwa nayo". Mwanjakwa (2024) anaeleza kuwa mawazo ya udhanaishi kuhusu kifo yanajidhihirisha pia katika methali na nahau zinazotumika nchini Malawi.

***Ukengeushi***

Ukengeushi ni hali ya mtengo au mbanduko au kuhisi ugeni. Ni hali ambayo mtu huamua kukiuka kaida na taratibu zilizowekwa. Kila jamii ina kaida na kanuni ambazo kila mwanajamii anapaswa kuzifuata, kuziishi na kuzizingatia. Kwa hiyo, katika utafiti huu tulibaini misemo ambayo inasawiri mawazo ya wadhanaishi katika mhimili huu. Tazama mifano katika jedwali lifuatalo:

*Jedwali Namba 4. Misemo Inayosawiri Ukengeushi*

| **Namba** | **Msemo** |
|---|---|
| 1. | Naishi nipendavyo si mtakavyo |
| 2. | Sheria si msahafu |
| 3. | Akili za kuambiwa changanya na za kwako |
| 4. | Anayekimbia kivuli chake hawezi kushinda |
| 5. | Sheria ziliwekwa ili zivunjwe |

**Chanzo:** *Data za Utafiti (Mei- Septemba, 2024)*

Mifano katika jedwali namba 4 inawasilisha misemo inayosawiri mhimili wa ukengeushi katika Nadharia ya Udhanaishi. Msemo *"Naishi nipendavyo si mtakavyo"* unabainisha kuwa, katika kupambana na maisha mtu huamua kufanya kile anachokiamini kuwa ndicho sahihi. Msemo huu unaonesha uhuru mbapo mtu hukiuka kaida za jamii kwa kuona hakuna mtu mwenye haki ya kuamua kuhusu maisha yake. Msemo *"sheria si msahafu"* huonesha kuwa sheria huweza kubadilishwa. Msahafu ni kitabu cha dini ya Kiislamu (Kuran), kinachoweka sheria, misingi na miongozo ya Uislamu na haibadiliki. Mtu anapokengeuka hutumia misemo inayompa nguvu ya kuona yupo katika njia iliyo sahihi. Misemo hii *"Naishi nipendavyo si mtakavyo*" na "*Sheria si msahafu"*. Aidha, msemo "akili za kuambiwa changanya na za kwako" unatoa funzo kuwa si kila ulilolekezwa kufanywa linapaswa kuwa sheria na kaida. Hivyo, mtu anapaswa kutumia akili zake katika kutenda na kuamua mambo. Msemo *"anayekimbia kivuli chake hawezi kushinda"* ina maana kwamba mtu ambaye haishi kwa misingi ya utu na uhalisia wake hawezi kufikia mafanikio. Misemo *"sheria ziliwekwa ili*

*zivunjwe"* unasisitiza kuwa katika jamii sheria na taratibu zipo ila haina maana kwamba lazima sheria hizo zifuatwe maana zipo ili zikiukwe na huo ndiyo uhalisia wa maisha katika jamii. Tariq (2017) anasema, Udhanaishi unapendekeza mwanadamu kujiamulia, na hawezi kufuata imani (simulizi kuu) au mkondo fulani wa mawazo isipokuwa atajifunga mwenyewe. Hata hivyo, katika uhuru huu yuko pweke kwani jukumu la kujitafutia maana ya maisha yake ni lake binafsi. Katika juhudi hizi, baada ya kujitenga na imani za kijadi zilizomweleza mwanadamu, anautazama ulimwengu kwa pazia ya utosahihi (inauthenticity), na anagundua ukweli kuhusu imani aliyokuwa nayo ya ulimwengu huu usio maana. Ni bayana kuwa misemo ya Kiswahili iliyojadiliwa inaambatana na mhimili wa ukengeushi kwa kumpa binadamu uhuru wa kupinga kaida za kijamii na kujiandalia njia mpya ya kimaisha, huku akijitahidi kutafuta uhuru na maana katika ulimwengu huu. Suala hili limejadiliwa pia na Akinola (2023) ambapo anasema Nadharia ya Udhanaishi inasaidia katika kupata uelewa mzuri wa chanzo cha uwepo wa binadamu na uhuru Afrika.

***Utamaushi***

Utamaushi ni hali ya kukata tamaa na kuona maisha hayana maana. Wadhanaishi wanaamini kwamba, ijapokuwa mwanadamu yuko huru kuamua na kuwa chochote anachotaka kuwa, anafaa kujua kuwa uhuru huu una mipaka hasa katika mapungufu ya kimaumbile (Akinbode, 2023; Akinola, 2023). Katika tafiti huu ulibaini kuwa kuna misemo ya Kiswahili ambayo inafungamana na mhimili wa Nadharia ya Udhanaishi kuhusu utamaushi. Tazama jedwali hapa chini:

*Jedwali namba 5: Misemo Kuhusu Utamaushi*

| Namba | Msemo wa Kiswahili |
|---|---|
| 1. | Maisha hayana maana |
| 2. | Maisha ni fumbo |
| 3. | Maisha ni mtihani |
| 4. | Maisha ni vita |
| 5. | Maisha ni safari |

***Chanzo:*** *Data za Utafiti (Mei- Septemba, 2024)*

Ukichunguza mifano katika jedwali namba 5 hapo juu utaona kuwa misemo ya Kiswahili katika jedwali hilo imefungamana na mhimili wa udhanaishi ambao unahoji kuhusu maana ya maisha na kuwako kwa binadamu. Wahojiwa walieleza kuwa msemo *"maisha hayana maana"* hutumika pale mtu anapokata tamaa ya maisha na kukosa sababu ya kuishi huku msemo *"maisha ni fumbo"* ukionesha kuwa hayapowazi, hayaeleweki. Misemo hii imefungamana na wazo la udhanaishi la kukata tamaa. Søren Kierkegaard katika kitabu chake *Fear and Trembling* (1941) anasema, "Kukata tamaa ni ugonjwa wa kifo, ni kutokuwa na uwezo wa kujipatanisha na upuuzi wa maisha na hisia ya kutengwa na ubinafsi wa kweli" (Egbekpulu, 2022). Misemo hii inaonyesha kutoridhika na hali ya kutafuta maana katika maisha, huku mtu akiona maisha ni mfumuko wa upuuzi na hayana maana.

Katika msemo *"maisha ni mtihani"* maisha yanafananishwa na mtihani unaobeba dhana ya kufaulu na kushindwa. *"Maisha ni vita"* ni msemo unaoyafananisha maisha na vita. Vita ni mapigano na mapambano ambapo kuna kushinda na kushindwa. Katika vita kuna taabu, shida, njaa, magonjwa, vifo na kila aina ya mateso. Hivyo, Waswahili huona maisha ni vita baina ya binadamu na maisha. Msemo wa Kiswahili *"maisha ni safari"* unayafasiri maisha kama harakati za safari za kutafuta ukweli na uzuri wa maisha. Binadamu anapoishi anapita katika njia mbalimbali zenye nyakati za furaha na huzuni nyingi. Misemo hii inasawiri mawazo ya ambaye anasisitiza kuwa maisha ni safari ya mtu binafsi, inayohitaji kukutana na hali ya upweke na kutokuwa na maana ya juu, na katika kutafuta maana ya maisha, mtu anahitaji kukabiliana na upweke huu (Heidegger, 2008). Hivyo, katika kusawiri maisha, jamii ya Waswahili hutumia misemo inayofungamana na udhanaishi kuhusu tafsiri

mbalimbali dhana ya maisha. Matokeo haya hayana tofauti na Akinola (2022) ambaye anaeleza kuwa udhanaishi utumika kuelezea dhana ya maisha katika jamii za Kiafrika na uwepo wa Mungu.

### *Kuabudu Mahitaji ya Kimwili*

Utafiti huu uligundua kuwa, katika Kiswahili kuna misemo ambayo imefungamana na Nadharia ya Udhanishi kuhusu kuabudu mahitaji ya kimwili. Tazama misemo katika jedwali namba 6:

*Jedwali Namba 6: Misemo inayosawiri Kuabudu Mahitaji ya Kimwili*

| Namba | Msemo |
|---|---|
| 1. | Mapenzi ni upofu |
| 2. | Maskini hapendeki |
| 3. | Mapenzi ni ajali |
| 4. | Kipendacho roho hula nyama mbichi |
| 5. | Mapenzi siyo pesa |

*Chanzo: Data za utafiti (Mei- Septemba 2024)*

Data ya misemo katika jedwali namba 6 inawasilisha misemo ya Kiswahili iliyofungamana na udhanaishi kuhusu kuabudu mahitaji ya mwili. Mfano, *"mapenzi ni upofu"* msemo huu unajenga dhana kwamba mtu akipenda haoni mapungufu ya anayempenda. Mtu anapokuwa katika mapenzi huhitaji kutimiza mahitaji yake ya kimwili bila kujali athari anayoipata. Katika misemo kama *"Kipendacho roho hula nyama mbichi"*, na *"nzi kufia kwenye kidonda"* tunapata wazo kwamba tamaa za kimwili zinaweza kumgharimu mtu kiroho na kimwili, na hivyo kuwa ni upofu wa roho ambayo inashindwa kutambua athari za tamaa hizi. Haya yanaambatana na mawazo ya Nietzsche (1883:23) katika Gödde na wenzake (2023) anaeleza kwamba "Mwili ni wenye sababu kubwa, lakini pia ni mdanganyifu, anayeijaribu nafsi kujiingiza katika tamaa zake. Na nafsi, ikiwa imewahi kuonja mwili, inajitahidi kujitenga na mshiko wa ulevi wa hisi" Hapa, Nietzsche anasisitiza kuwa mwili unatawaliwa na tamaa, huku binadamu akishindwa kutafuta ukweli kuhusu maana ya maisha yake.

## Hitimisho

Makala hii ilichunguza usawiri wa Nadharia ya Udhanaishi katika misemo ya Kiswahili, ikitumia mihimili sita ya udhanaishi. Matokeo ya utafiti yamedhihirisha kuwa udhanaishi ni falsafa ya maisha ya kila siku ya binadamu, na misemo ya Kiswahili inasawiri Udhanaishi kwa kujikita katika masuala mbalimbali kama vile uhuru binafsi, uwepo wa Mungu, kifo, maana ya maisha, ukengeushi na kuabudu mahitaji ya kimwili. Utafiti huu unatoa mchango muhimu kwa kuelewa jinsi misemo ya Kiswahili inavyoweza kutumika kama nyenzo ya kuelezea Nadharia ya Udhanaishi na vile vile jinsi inavyoakisi falsafa za maisha ya kila siku katika jamii ya Waswahili.

## Marejeo

Akinola, F. A. (2022). Existentialism and the African Nature of Man: interrogating the Concept of Better Human Existence in Africa. *Human Discourse*, *2(1)*, 1-6.

Akinola, F. A. (2023). An African Appraisal of Sartre's Existentialism and its Implications for Human Existence in Africa. Ochendo: *An African Journal of Innovative Studies*, *4(1)*, 97-111.

Akinbode, E. (2023). Jean Paul Sartre's Existential Freedom: A Critical Analysis. *International Journal of European Studies*, *7*(1), 15-18.

Beauvoir, S. de. (2018). *The Ethics of Ambiguity* (B. Frechtman, Trans.). Open Road Media. (Original work published 1947).

Camus, A. (1955). *The Myth of Sisyphus, and Other Essays.* Knopf.

Copper, D. (1990). *Existentialism*. Blackwell Publishers.

Earnshaw. S. (2006). *Existentialism: A Guide for the Perplexed*. Continuum International Publishing Group.

Egbekpulu, P. E. (2022). A Comparative Analysis of Kierkegaardian and African Existentialism. *International Journal of Research and Innovation in Social Science*, *VI*(III), 261-265.
Etta, E. E., & Mogu, I. F. (2012). The Relevance of Proverbs in African Epistemology. *A Journal of Contemporary Research*, *9(1)*, 186-205.
Flynn, T. R. (2006). *Existentialism: An Introduction*. Oxford University Press.
Gödde, G., Z., J., Mueller, R. G., & Stegmaier, W. (Eds.). (2023). *Nietzsche on the art of living: New studies from the German-speaking Nietzsche research*. Orientations Press LLC.
Heidegger, M. (2008). *Being and Time*. Harper Collins.
Jha, K. B. (2020). Features of Existentialism. *Journal of Humanities and Social Science*, *25(8)*, 60-63.
Kierkegaard, S. (1941). *Fear and Trembling*. Princeton University Press.
Kierkegaard, S. (1983). *Fear and Trembling*. (Tr. Howard V. Hong and Edna H. Hong). Princeton University Press.
Kierkegaard, S. (1993). *Upbuilding discourses in various spirits* (Howard & E. Hong, Trans.). Princeton University Press.
Kierkegaard, S. (1997). Christian Discourses. Translated by Howard V. Hong and Edna H. Hong: Princeton University Press.
Kipacha, K. (2014). Misemo Katika Lugha za Magari: Divai Mpya? *Swahili Forum*, 21, 104-121
Kipacha, A. (2019). "Kifo au Maisha ya Maumivu: Usomaji wa Rosa Mistika ya Euphrase Kezilahabi kwa Jicho la Kikanushi". Katika A.S. Ponera na Z.A. Badru, (Wah.) Koja la *Taaluma za Insia: Kwa Heshima ya Prof. Madumulla*. Karljamer Publishers Ltd. pp. 422-434.
King'ei, K. & Ndalu A. (2007). *Kamusi ya Semi (Toleo Jipya)*. East African Educational Publishers.
Fuluge, A. (2022). Matukio ya Mchakato wa Kujiua katika Riwaya ya Rosa Mistika. *Mulika*, *41(2)*, 145-1611.
Fuluge, A. (2024). Mitanziko ya Wahusika katika Riwaya Teule za Euphrase Kezilahabi. *Kioo cha Lugha*, *22(1)*, 90-111.
Gaudioso, R. (2014). Kuwako na Wakati: Mipaka ya Lugha kama Hatua za Falsafa katika Mashauri ya Euphrase Kezilahabi. *Swahili Forum, 21,* 76-103.
Gaudioso, R. (2015). "Transferring and Rewriting Freedom in Euphrase Kezilahabi". *Nordic Journal of African Studies*, *23*(2), 63−89.
Moore, C. E. (Ed.). (2002). *Provocation: Spiritual writings of Kierkegaard* (p. IX). Retrieved from https://www.sorenkierkegaard.nl/artikelen/Engels/187.%20Provocations.pdf
Mulokozi, M. (1996). *OSW 105: Fasihi ya Kiswahili*. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
Mulokozi, M. M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. KAUTTU.
Mwanjakwa, M. D. (2024). Why are We here? Existentialism in local Malawian lore. *J. Hum*, 32(2), 116-140.
Njogu, K., & Chimera, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Jomo Kenyatta Foundation.

Rehak, V. (2007). Kazimoto and Meursault: Brothers in Despair and Loneliness, Comparing Kezilahabi's *Kichwamaji* and Camus' *L'Estranger*, *Swahili Forum*, 14, 13−51.
Rettová, A. (2016). Existentialism and Swahili Literature. Katika Abdilatif abdalla: *Poet in Politics.* 109-122. Mkuki na Nyota.
Reynolds, J. (2006). *Understanding Existentialism.* Acumen Publishing Print.
Sartre, J. P. (1947). *Existentialism.* Trans. by Bernard Reidman. Philosophical Library
Sartre, J. P. (1957). *The Humanism of Existentialism.* In C. G. Guignon& D. Pereboom (2.), Existentialism Basic Writings (pp. 290-308). (B, Frechtman, Trans.). Indianapolis, IA: Hackett. P296.
Sartre, J. P. (2008). *Being and Nothingness*. Routledge.

Sartre, J. P. (2018). *Being and nothingness: An essay in phenomenological ontology* (S. Richmond, Trans.). Routledge. https://doi.org/10.4324/9780429434013

Sasan, M. J. (2023). Existentialism and Its Influence on Our Understanding of Knowledge, Truth, Morality, Values, and Religion. *European Journal of Learning on History and Social Sciences*, *1*(1), 40-51.

Sherman, D. (2007). *Camus* (p. 71). John Wiley & Sons, Ltd.

Suastra, A. W., Tungga, W. A. & Tika, I. N. (2024). An Existentialism Approach to Language and Literature Education to Build Student Personality. *Jurnal Pendidikan Mandala*, *9*(4), 1216-1224.

Tariq, U. (2017). "Exploring Existentialism in Postcolonial Literature through Salman Rushdie's 'Midnight's Children'". Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Greenwich, bewa la Karachi, Pakistani (Haijachapishwa).

Wafula, R. na K. Njogu (2007). *Nadharia na Uhakiki wa Fasihi.* Chuo Kikuu cha Jomo Kenyatta.

Wamitila, K. (2003). *Kichocheo cha Fasihi: Similizi na Andishi*. Focus Books.

Wanjala, F. S. (2011). *Kitovu cha Fasihi Simulizi kwa Shule, Vyuo na Ndaki*. Serengeti Publishers.